

**OFISI YA WAZIRI MKUU  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**WILAYA YA BIHARAMULO**

**TAARIFA YA MAFANIKO YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE KWA  
KIPINDI CHA MIAKA 10 KUANZIA MWAKA 2005 HADI JUNI 2015**



**Ofisi ya Mkuu wa Wilaya  
S. L. P 21  
SIMU: 028-2225002  
FAX : 028-2225216**

**Juni, 2015**

## YALIYOMO

1. UTANGULIZI.....	3
2. HISTORIA YA WILAYA YA BIHARAMULO.....	3
3. JIOGRAFIA YA WILAYA.....	4
4. HALI YA HEWA.....	4
(i) Kanda ya Magharibi.....	4
(ii) Kanda ya Kusini.....	4
(iii) Kanda ya Mashariki:.....	4
5. ENEO LA WILAYA.....	5
5.1 UTAWALA.....	5
5.2 IDADI YA WATU.....	5
6 SHUGHULI ZA KIUCHUMI.....	5
<b>UTEKEZAJI WA ILANI KISEKTA</b>	
7 SEKTA ZA UZALISHAJI.....	6
7.1 KILIMO.....	6
7.2 MIFUGO.....	10
7.3 UVUVI.....	12
7.4 USHIRIKA NA SACCOS.....	12
8 MIKOPO YA WANAWAKE NA VIJANA.....	13
8.1 Mikopo kwa wanawake.....	13
8.2 MIKOPO KWA VIJANA.....	14
9 ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA.....	14
10 ELIMU.....	15
10.1 Elimu ya Awali:.....	15
10.2 Elimu ya Msingi:-.....	16
10.3 Elimu ya Sekondari:.....	19
10.4 Ufaulu wa Mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha Pili mwaka 2005 - 2015.....	19
10.5 Ufaulu wa Mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha Nne mwaka 2005-2015.....	20
10.6 Elimu ya Ualimu:-.....	21
10.7 Elimu ya Ufundi:-.....	21
11 AFYA.....	21
11.1 Chanjo za watoto chini ya mwaka mmoja zimeongezeka kama ifuatavyo:-.....	22
11.2 Upatikanaji wa Dawa na Vifaa vya Tiba.....	24
11.3 UKIMWI.....	24
12 Ustawi wa Jamii.....	24
12.1 Ukomeshaji wa ajira kwa watoto.....	24
12.2 Watoto walemavu.....	25
12.3 Watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi.....	25
12.4 Wazee.....	26
13 MAJI:.....	27
13.1 Huduma ya Maji Safi na Usafi wa mazingira.....	27
14 MIUNDOMBINU:.....	29
14.1 Sekta ya Barabara.....	29
14.2 UMEME:.....	32
14.3 Umeme.....	32
14.4 Mawasiliano ya Simu.....	33
15 UKUSANYAJI WA MAPATO:.....	33
16 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUITATUA.....	35

# **TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE KWA KIPINDI CHA MWAKA 2005 HADI MWEZI JUNI, 2015**

## **1. UTANGULIZI**

Katika kipindi hiki cha miaka kumi Halmashauri ya Wilaya iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira, Dhima na Mikakati mbalimbali iliyojiwekea kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005-2010 hadi 2010-2015. Ilani ya CCM inabainisha kwamba kilimo cha kisasa ndio msingi na sharti muhimu katika kujenga uchumi wa kisasa na kina nafasi ya kimkakati katika modenaizesheni ya uchumi wa Tanzania.

Serikali ya awamu ya nne imeendeleza kwa nguvu zote juhudi za kupambana na maadui wakuu watatu, maradhi, ujinga na umaskini, kwa kushirikiana na wafadhili, sekta binafsi na jamii kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupambana na Umaskini (MKUKUTA), Malengo ya Maendeleo ya Millennia (MGDs) na kwa kuzingatia utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa sasa (BRN) ambayo imeipa kipaumbele sekta ya Afya, Maji, Miundombinu, Kilimo, Elimu na Mapato

Halmashauri ya wilaya ya Biharamulo kwa upande wake imesimamia na kutekeleza maelekezo na program mbalimba ili kuhakisha kuwa matokeo makubwa yanapatikana katika sekta zote ili hatmae kuwaletea wananchi maendeleo na Taifa kwa ujumla

Juhudi kubwa zimefanyika ili wananchi wa wilaya hii waweze kuelewa na hatimaye washiriki kikamilifu katika utekelezaji na usimamizi wa wa shughuli zao za maendeleo ili ziwe na matokeo chanya

## **2. MIPAKA YA WILAYA.**

Wilaya hii ilianzishwa rasmi mwaka 1961 na Halmashauri iliundwa mwaka 1983 na kuanza shughuli zake mwaka 1984. Wilaya ya Biharamulo ni mojawapo kati ya Wilaya saba (7) za Mkoa wa Kagera. Wilaya inapakana na Wilaya za Muleba na Karagwe kwa upande wa Kaskazini, Wilaya za Kakonko na Bukombe upande wa Kusini, Wilaya ya Ngara upande wa Magharibi na Wilaya ya Chato upande wa Mashariki.

### **3. JIOGRAFIA YA WILAYA.**

Wilaya ipo kilomita 171 kutoka Manispaa ya Bukoba – ambayo ni Makao Makuu ya Mkoa wa Kagera. Wilaya inapatikana kati ya nyuzi 2° 15’ – 3° 15’ Kusini mwa Ikweta na 31° – 32° Mashariki mwa “Standard Meridian”.

### **4. HALI YA HEWA**

Hali ya hewa kwa ujumla ni joto la wastani wa 27° C. Kijiografia Wilaya ya Biharamulo imegawanyika katika kanda kuu tatu za hali ya hewa ambazo ni Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kusini na kanda ya Mashariki kama ifuatavyo:

#### **(i) Kanda ya Magharibi**

Kanda hii ina mwinuko wa kati ya mita 1250 – 1400 toka usawa wa bahari. Kanda Hii inapata kiasi cha mvua kati ya 800mm – 1000mm na ina udongo wa kichanga aina ya “Bukoba sandstone”. Mazao yanayolimwa ni Migomba, mahindi, mtama, mpuga na muhogo. Tumbaku na Kahawa ni mazao makuu ya biashara katika kanda hii. Kanda hii inajumuisha kata za Nyarubungo, Biharamulo Mjini, Ruziba, Bisibo na Nyamahanga.

#### **(ii) Kanda ya Kusini**

Kanda hii ina mwinuko kati ya mita 1200 – 1,700 toka usawa wa bahari ambao kwa sehemu kubwa ni misitu ya hifadhi ambayo hupata mvua za kiasi cha milimita 700 – 850. Mazao yanayostawishwa katika kanda hii ni Kahawa, Tumbaku, Mihogo, Viazi Vitamu, mahindi, mtama na Maharage. Mazao mengine ya misitu hupatikana katika ukanda huu ikiwa ni pamoja na asali, mbao na mkaa. Kanda hii inajumuisha kata za Kalenge, Lusahunga, Nyakahura Nyantakara na Kaniha.

#### **(iii) Kanda ya Mashariki:**

Kanda hii ina mwinuko kati ya mita 1100 mpaka 1400 kutoka usawa wa bahari. Kanda hii inapata kiasi cha mvua kwa wastani kati ya 800mm - 900mm kwa mwaka na ina udongo wa kichanga na mbuga.

Mazao yanayolimwa katika kanda hii ni muhogo, mahindi, mpunga, mtama, karanga na maweale. Mazao makuu ya biashara ni pamba, kahawa na tumbaku. Kanda hii inajumuisha Kata za Runazi, Kabindi, Nyamigogo Nemba na Nyabusizi.

## **5. ENEO LA WILAYA**

Wilaya ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 5,627 kati ya eneo hilo, kilometa za mraba 5,617 ni nchi kavu na kilometa za mraba 10 ni eneo la maji. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 253,215.

### **5.1 UTAWALA**

Maeneo ya utawala yameongezeka kutoka tarafa 2, Kata 8, Vijiji 49 na vitongoji 299 mwaka 2005 hadi tarafa 2, Kata 17, Vijiji 80 na Vitongoji 402. (zimeongezeka kata mbili za Katahoka na Nyanza ambazo zitaongeza idadi ya waheshimiwa Madiwani baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2015). Kati ya vitongoji hivyo, Mamlaka ya Mji mdogo wa Biharamulo una jumla ya vitongoji 5. Wilaya ina jimbo moja la uchaguzi la Biharamulo. Kwa upande wa uwakilishi wa wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ina jumla ya Madiwani 21 kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi	1
Waheshimiwa Madiwani wa Kuchaguliwa, Kata	15
Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalumu	5

### **5.2 IDADI YA WATU**

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2012, Wilaya ilikuwa na watu 323,486, wanaume 160,572 na wanawake 162,914, kwa sasa Wilaya inakadiriwa kuwa na watu 354,541 wanaume 175,994 na wanawake 178,547 hii ni kutokana na ongezeko la asilimia 4.8 kwa mwaka. Idadi ya kaya nayo imeongezeka toka kaya 53,914 mwaka 2012 hadi kaya 59,090 mwaka 2015.

## **6 SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

Juhudi zinaendelea kufanyika katika sekta kuu za uzalishaji, huduma za jamii na sekta za kiuchumi ili kuboresha hali ya maisha ya Wananchi. Zaidi ya asilimia 85% ya wakazi wa Wilaya ya Biharamulo hutegemea kilimo kwa kujiongeza kipato, ambapo hutegemea sana mauzo kutokana na mazao makuu ya kilimo ambayo ni Pamba, Tumbaku, Kahawa, Mihogo, Mahindi na Mpunga.

Mifugo na mazao yake hutegemewa pia na wakazi wa Wilaya hii na asilimia 15.4% ya kaya zote za wilaya hii zinafuga mojawapo ya wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Mchango wa kila sekta katika maendeleo ya uchumi ni kama ifuatavyo; Kilimo 85%, shughuli za biashara 5% watumishi (kazi za ofisini ) 1.6%, ufugaji 7% na shughuli nyingine ndogo ndogo 1.4%

# UTEKELEZAJI WA ILANI KISEKTA

## 7 SEKTA ZA UZALISHAJI

### 7.1 KILIMO

**Maelekezo ya Ilani;** kutekeleza kwa ukamilifu malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) pamoja na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Kilimo ndiyo msingi wa uchumi wa kisasa na njia sahihi ya kuutokemeza umaskini. Kilimo kimeendelea kuwa uti wa mgongo kwa wilaya ya Biharamulo

#### **Mafanikio:**

- Watumishi wa kilimo (ugani) wameongezeka kutoka watumishi 20 mwaka 2005 hadi watumishi 58 mwaka 2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 66. Kwa sasa idara ina mahitaji ya watumishi 45 sawa na asilimia 44.
- Uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula umeongezeka kutoka tani 160,768 mwaka 2005 hadi tani 379,804 mwaka 2015; sawa na ongezeko la asilimia 136. Ongezeko hili linatokana na pembejeo za ruzuku iliyotolewa na Serikali.
- Tija ya uzalishaji wa mazao makuu umeongezeka katika kipindi cha miaka kumi (2005 hadi 2015) kama ifuatavyo:

#### **Jedwali namba 1 uzalishaji wa mazao makuu**

<b>Na</b>	<b>Zao</b>	<b>Tija mwaka 2005 (Tani kwa Ha.)</b>	<b>Tija mwaka 2015 (Tani kwa Ha.)</b>	<b>Ongezeko (%)</b>
1	Mahindi	1.2	1.7	41.67
2	Muhogo	7	15	114.29
3	Maharag e	0.45	0.8	77.78
4	Ndizi	8	20	150.00
5	Pamba	0	0.9	-
6	Tumbak u	0.6	1.7	183.33
7	Kahawa	0.25	0.7	180.00

Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

## Kilimo cha zao la ndizi Wilayani Biharamulo



- Ongezeko hili limetokana na matumizi ya mbolea ambayo yameongezeka kutoka tani **0.003** kwa hekta mwaka 2005 hadi **0.017** mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia **3.25** Ongezeko hili linatokana na pembejeo za ruzuku iliyotolewa na serikali.
- Mbolea ya Ruzuku imeongezeka kutoka tani **0** mwaka 2005 hadi tani **1,250** mwaka 2015. Wilaya iliingia kwenye mfumo wa upatikanaji wa Pembejeo za Ruzuku ya serikali mwaka 2012/2013.
- Matumizi ya wanyamakazi katika kilimo yameongezeka kutoka asilimia **1.7** mwaka 2005 hadi **5** mwaka 2015.
- Matumizi ya mbegu bora yameongezeka kutoka tani **0.56** mwaka 2005 hadi tani **105** mwaka 2015 sawa na asilimia **18,650%**. Ongezeko hili linatokana na pembejeo za ruzuku iliyotolewa na Serikali pamoja na uhamasishaji wananchi juu ya matumizi ya mbinu bora za kilimo

### Jedwali Na. 2: Matumizi ya vocha za pembejeo msimu wa mwaka 2013/14

Aina ya Pembejeo	Mgao wa Vocha	Thamani ya kila vocha	Thamani (Tshs)	Wakulima walionufaika	Kiasi cha Tani	Vocha Salia	% ya Usamaji
Mbolea za kupandia	4,965	50,000	250,000,000	3,437	248.25	1,528	69.2
Mbolea za kukuzia	4,965	40,000	200,000,000	3,437	248.24	1,528	69.2
Mbegu za Mahindi (OPV)	4,965	10,000	50,000,000	3,437	49.65	1,528	69.2
<b>Jumla</b>			<b>500,000,000</b>	<b>3,437</b>	<b>334.9</b>	<b>1,528</b>	<b>69.2</b>

**Chanzo: Mkurugenzi Mtendaji (W)**

- Wilaya imeweza kudhibiti hali ya maambukizi ya ugonjwa wa Mnyauko wa Migomba (unyanjano) hadi kufikia mwezi Juni, 2015 Jumla ya migomba 41,095 iliyobainika kuambukizwa na kuugua iliteketezwa. Kwa sasa hakuna tatizo la ugonjwa huu kwa Wilaya hii.
- Matumizi ya matrekta madogo yameongezeka kutoka matrekta **2** mwaka 2005 hadi matrekta **15** mwaka 2015 sawa na asilimia **650**.
- Matumizi ya Matrekta makubwa yameongezeka kutoka matrekta **2** mwaka 2005 hadi matrekta **9** mwaka 2015 sawa na asilimia **350**
- Wilaya hadi sasa haina mradi wa kisasa wa Kilimo cha umwagiliaji, umwangiliaji unaofanyika ni wa asili katika mashamba ya mpunga. Eneo linalofaa kwa umwangiliaji ni hekta 2400 ambazo zinategemewa kutoa uzalishaji wa tani 6,400 baada ya mradi wa umwagiliaji wa bonde la mto Mwiruzi kujengwa.

## **ZAO LA MNYORORO WA THAMANI**

Katika mpango wa serikali wa kuhakikisha ruzuku ya serikali katika kuendeleza Sekta ya Kilimo katika mipango ya Kilimo ya Wilaya (**DADPs**) inatumika kwa namna ambayo italetwa matokeo yanayotrajiwa, mwaka 2012/2013 ilianzisha utaratibu wa kila wilaya kuwa na zao moja ambalo litapata ruzuku ya serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo katika wilaya husika kwa hatua zote kuanzia uzalishaji, usindikaji hadi masoko.

Utaratibu wa kupata zao husika kwa kila Wilaya ulihusisha wadau mbalimbali ndani ya Wilaya kwa kuainisha mazao yote makubwa yanayolimwa katika wilaya husika na baada ya mchakato mrefu wa majadiliano na uchambuzi wa kina wa kila zao wadau wanafikia makubaliano ya pamoja na kupata muafaka wa kuwa na zao husika.

Kwa kufuata utaratibu huu Wilaya ya Biharamulo ilichagua zao la Muhogo kuwa ndio lipewe kipaumbele cha kuwekwa katika utaratibu wa mnyororo wa thamani. Hii ilitokana na ukweli kuwa zao hili linalimwa na asilimia kubwa ya wakulima na wakazi wa Wilaya hii, aidha ni zao ambalo soko lake ni kubwa ndani na nje ya wilaya na hata nje ya mipaka nchi katika nchi za Burundi, Rwanda, Kongo na Uganda ambako huuzwa kama mhogo mkavu ambao haujasindikwa ujulikanao kama “Makopa”. Hivyo wilaya iliona ni vema zao hili lihudumiwe katika hatua zake zote



kuanzia uzalishaji, mafunzo kwa wakulima, usindikaji na upatikanaji wa masoko.

Zao hili lilianza kuhudumiwa kwa mfumo huu toka mwaka 2013/2014 na mwaka 2014/2015 ulikuwa mwaka wa pili wa utekelezaji wa mfumo huu. Kwa kipindi hiki cha miaka miwili wakulima 540 kutoka kwenye vikundi 12 katika vijiji 12, ambapo kila mkulima ameweza kupatiwa mbegu pingili 4,000 inayotosha ekari 1. Mbegu waliopatiwa ni aina ya **MKOMBOZI** na **MEREMETA** ambazo huzalishwa na vituo vya utafiti kwa ajili ya kukabiliana au kukinzana na matatizo ya magonjwa ya muhogo ya **BATOBATO** na **MCHIRIZI KAHAWIA**.

Aidha vikundi hivyo vimepatiwa mashine za kusaga nafaka 12 ambapo kila kikundi kimepatiwa mashine moja na Vikundi 6 vya mwaka 2013/2014 vilipatiwa mashine 12 za kuchakata muhogo (Cassava press mashine 6 & Cassava grater mashine 6). Kikundi kimoja cha Mihongora kimeweza kupatiwa trekta moja na zana zake ambazo ni jembe la plau, haro na tela.

Wilaya inashirikiana na wadau 4 wa maendeleo ambao ni Uliokuwa Mgodini wa dhahabu wa TULAWAKA na sasa STAMIGOLD, RUDDO/CONCERN, MEDA, na COVER. Wadau hao wamechangia kuendeleza zao la muhogo kama ifutayvo

- Mgodini wa dhahabu wa **TULAWAKA** (kwa sasa unajulikana kama STAMIGOLD). Mgodini ulisaidia mashine 4 za kuchakata muhogo kwa vikundi 2 vya Kijiji cha Mavota na kugharamia mafunzo ya usindikaji wa zao la muhogo kwa kutumia mashine walizopewa kwa wanakikundi wakulima wapatao ishirini (20). Pia kila mkulima alipatiwa mbegu ya muhogo kiasi cha pingili 4,000 inayotosha ekari moja.
- **RUDDO/CONCERN** wamesaidia mashine seti 6 za kusindika muhogo kwa wajasiriamali 6 katika vijiji vya Kalenge, Isambara, Mihongora, Kasato, Nyantakara na Katahoka. Aidha wamefadhili ujenzi wa majengo 6 ya mashine hizo kwa zaidi ya asilimia 75. Vilevile wanategemea kutoa mashine nyingine mbili kabla ya mwezi Desemba 2015 kwa wajasiriamali wengine wawili wa vijiji vya Kagondo na Kikomakoma ikiwa ni pamoja na ujenzi wa majengo ya mashine hizo.
- **MEDA** (Taasisi isiyokuwa ya Kiserikali) inayojihusisha na uzalishaji wa mbegu bora za muhogo inayokinza na magonjwa mbalimbali ya muhogo ambayo inafanya kazi katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Tanga na Dodoma na sasa wameweza kufika katika baadhi ya Wilaya Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Biharamulo ikiwa mojawapo. Taasisi hii inafadhiliwa na Bill and Melinda Gates. Kutokana na ufadhili wa taasisi hii mpaka sasa maandalizi ya mashamba mawili ya mbegu ya msingi

yameandaliwa katika vijiji vya Kagondo shamba la ekari 3 na Nyakahura shamba la ekari 3. Mashamba haya yatakuwa na uwezo wa kuzalisha pingili 40,000 kwa ekari. Maafisa ugani 2 wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji bora wa mbegu huko Bunda. Mashamba 9 ya mfano yataanzishwa katika vijiji vya Kagondo, Nyakahura, Nyabusozzi, Isambara na Mihongora mashamba matano (5).

- **Shirika la COVER** ambalo lilihusika kutoa mafunzo kwa Maafisa wawili kutoka Makao Makuu ya Idara na wajasiliamali 24. Mafunzo haya yalibusu Usindikaji (Processing), Ufungashaji (Packaging) na Maswala ya Masoko (Marketing).

## **7.2 MIFUGO**

Katika mkakati wa kuboresha uzalishaji na mchango wa sekta ya mifugo kwenye pato la taifa, msukumo ni kuongeza uzalishaji na ubora kuliko uwingi wa mifugo kwa eneo

### **Mafanikio;**

- Idadi ya wataalamu wa mifugo wameongezeka kutoka watumishi **7** mwaka 2005 hadi watumishi **14** mwaka 2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia **100**. Kwa sasa idara ina mahitaji ya watumishi 45
- Dawa za kuogeha mifugo zenye Ruzuku ya Serikali zimeongezeka kutoka lita **0** mwaka 2005 hadi lita **1,800** mwaka 2015. Uogeshaji huo umewezesha kupunguza vifo vitokanavyo na magonjwa ya kupe kutoka asilimia **21** mwaka 2010 hadi asilimia **12** Machi, 2015
- Idadi ya Wataalamu waliopatiwa mafunzo ya uhamilishaji (Artificial Insemination) imeongezeka toka **0** mwaka 2005 na kufikia **4** mwaka 2015.
- Ng'ombe waliohamilishwa wameongezeka toka **0** mwaka 2005 hadi **154** mwaka 2015 na tayari ng'ombe chotara **116** wamezaliwa.
- Elimu kupitia mashamba darasa ya ufugaji imeongezeka kutoka Mashamba darasa **0** mwaka 2005 hadi **34** mwaka 2015.
- Idadi ya wafugaji waliopata mafunzo ya ufugaji bora imeongezeka toka **208** mwaka 2005 hadi **1,020** sawa na ongezeko la asilimia **292.3**
- Malambo ya maji yakunywesha mifugo yameongezeka toka malambo **2** mwaka 2005 hadi malambo **7** mwaka 2015 sawa na asilimia **250**.
- Idadi ya Minada imeongezeka toka **1** mwaka 2005 hadi **4** mwaka 2015 ambayo imewawezesha wafugaji kuuza mifugo yao kwa urahisi. Aidha,

wastani wa ng'ombe **21,033** huuzwa kwa mwaka na kuwaingizia wafugaji wastani wa Tsh. **8,413,200,000**.

- Ng'ombe wa maziwa wamepungua toka 378 mwaka 2005 hadi kufikia 234 mwaka 2015 sawa na asilimia 38.1 hii imetokana na wafugaji wengi kuuza mifugo yao kutokana na idadi ya wafugaji wengi kupata elimu ya ufugaji wa kisasa unaohamasishajamii kuwa na idadi ndogo ya mifugo na wenye tija .
- Vifo vya ndama kabla ya kufikia mwaka mmoja kutokana na magonjwa yaenezwayo na kupe vimepungua toka asilimia **34** mwaka 2005 hadi **12** mwaka 2015.
- Mbwa waliochanjwa dhidi ya kichaa cha mbwa wameongezeka toka mbwa **670** mwaka 2005 hadi kufikia mbwa **2,314** hadi mwezi Desemba 2014. Sawa na ongezeko la asilimia **245** na matukio ya watu kuumwa na mbwa wanaosadikika kuwa na kichaa cha mbwa umepungua hadi kufikia 2 kwa mwaka 2015
- Ng'ombe waliochanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu wamepungua kutoka **20,493** mwaka 2005 hadi kufikia **9,493** mwaka 2015.
- Ukusanyaji wa mapato yatokanayo na minada ya mifugo yameongezeka kutoka Tshs. **1,600,000/=** mwaka 2005 hadi Tshs **111,461,000** mwaka 2015. Mapato haya ni kwa Halmashauri na Serikali Kuu sawa na ongezeko la Tshs. **109,861,000/=**

Takwimu za mifugo iliyopo katika Wilaya yetu ya Biharamulo ni kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

**Jedwali Namba 3: Takwimu za Mifugo kuanzia mwaka 2005-2015**

<b>AINA YA MIFUGO</b>	<b>IDADI YA MIFUGO MWAKA 2005</b>	<b>IDADI YA MIFUGO MWAKA 2015</b>
Ng'ombe wa asili	99,018	100,502
Ng'ombe wa maziwa	1,106	234
Mbuzi wa asili	97,994	49,470
Mbuzi wa maziwa	265	0
Kondoo	11,089	4,742
Nguruwe	256	686
Kuku wa asili	101,081	70,940
Kuku wa mayai	426	1,964
Bata	33,693	2,192
Sungura	719	209

Mbwa	5,413	3237
Punda	211	61
Paka	3,064	1,217

\*\*\* Mwaka 2005 Halmashauri ilikuwa imungana na Chato\*\*\*

### Chanzo: Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

#### 7.3 UVUVI

##### Mafanikio:

- Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo haina shughuli za Uvuvi unaofanywa kwenye maziwa na mito, uvuvi uliopo ni wa Mabwawa
- Mwaka 2005 kulikuwa na mabwa **12** ambayo yalikuwa yazalisha kg **2400** za samaki na mwaka 2015 Wilaya ina jumla ya mabwa **24** kati ya hayo mabwawa **6** yanamilikiwa na vikundi ambayo yamezalisha kg **3,800** za samaki.
- Elimu kuhusu ubora na uhifadhi mzuri wa samaki imetolewa kwa vikundi **6** vya wafugaji wa samaki.

#### 7.4 USHIRIKA NA SACCOS

##### Mafanikio:

- Idadi ya vyama vya Ushirika vya Akiba na mikopo (SACCOS) vimeongezeka kutoka vyama **10** mwaka 2005 hadi **30** mwaka 2015 sawa na asilimia **200**.
- Idadi ya wanachama imeongezeka kutoka **2,507** mwaka 2005 hadi **6,714** mwaka 2015 kati yao wanawake ni **1,435** na wanaume ni **5,279** sawa na ongezeko la asilimia **168**.
- Mtaji umeongezeka kutoka sh. **106,236,000/=** mwaka 2005 hadi kufikia Tsh. **1,657,813,000/=** mwaka 2015; hii ikiwa sawa na ongezeko la Tsh. **1,551,577,000/=** sawa na asilimia **1461** Ongezeko hili limesaidia sana kubadili maisha ya wanachama.
- Kwa mwaka 2005 jumla ya SACCOS **3** zilipata mikopo yenye thamani ya Tsh **945,000** na mwaka 2015 SACCOS **6** zimepata mkopo wenye thamani ya Tshs **12, 069,029,000/=** asilimia **85.8%** imerejeshwa. Kiasi cha sh **1,713,818,000/=** hakijarejeshwa bado kipo katika mzunguko wa biashara na kipo ndani ya muda wa marejesho.

- Jumla ya wajasiriamali **2,515** walipata mkopo wa Tshs. **1,157,221,000/=** (kutoka kwenye mabanki na taasisi za fedha wakiwemo wanaume **1,121** na wanawake **809** ( watu Binafsi **1,930** na vikundi **77** vyenye jumla ya watu **585**). Mikopo hii iliongeza ajira kwa watu **2,515** wakiwemo wanaume **1,025** na wanawake **1,490**.
- Idadi ya vyama vya ushirika vya mazao vimeongezeka kutoka vyama **8** mwaka 2005 hadi vyama **11** mwaka 2015 sawa na asilimia **120**

## 8 MIKOPO YA WANAWAKE NA VIJANA

### 7.3 Mikopo kwa wanawake

Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilianza kutoa mikopo ya wanawake na vijana kuanzia mwaka 2004. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 ilitoa mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana Tshs. **8,000,000/=**. Hadi kufikia mwaka 2015 Halmashauri ya Wilaya imechangia na kuvikopesha vikundi vya wanawake kiasi cha Tsh **60,874,000/=** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ikilinganishwa na Tsh **8,000,000/=** zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka 2005.

**Jedwali Na 4: Mikopo ya wanawake na vijana 2005 – 2015**

MWAKA	IDADI YA VIKUNDI	IDADI YA WATU WALIO NUFAIKA	THAMANI YA MIKOPO (TSHS)	FEDHA ZILIZORE JESHWA	BAKI	MAELEZO
2005/06	16	196	-	-	-	
2006/07	73	318	-	-	-	
2007/08	72	357	8,000,000	8,000,000.00	-	
2008/09	40	234	-		-	
2009/10	35	196	13,000,000	13,000,000.00	-	
2010/11	45	372	-	-	-	
2011/12	71	440	-		-	Madeni
2012/13	84	743	27,830,000	26,200,000	1,630,000	yanafuatiliwa
2013/14	62	502	24,501,400	22,021,050	2,480,350	Wanaendelea kurejesha.
2014/15	8	87	13,300,000.00	0	13,300,000	
<b>JUMLA</b>	<b>498</b>	<b>3,358</b>	<b>86,631,400.00</b>	<b>69,221,050.00</b>	<b>17,410,350.00</b>	

**Chanzo: Mkurugenzi Mtendaji (W)**

## **8.2 MIKOPO KWA VIJANA**

Mikopo ya vijana imeongezeka kutoka 0 mwaka 2005 hadi kufikia Tsh. 22,274,000/= mwaka 2015

### **CHANGAMOTO**

Baadhi ya wakopaji hawarejeshi kwa wakati jambo linalopelekea kufikishwa mahakamani.

### **UTATUZI**

Msisitizo umekuwa ukiwekwa kwa SACCOS/Vikundi vinavyopewa mikopo kurejesha kwa wakati na kuheshimu masharti ya mkopo ili kuwezesha SACCOS zingine pamoja na vikundi kuendelea kukopa.

Halmashauri ya Wilaya katika bajeti ya mwaka 2015/16 imetenga kiasi cha Tshs. 45,647,600/= kwa ajili ya mikopo ya vikundi vingine vya wanawake, lengo likiwa ni kuviwezesha vikundi vingi zaidi kufaidika na utaratibu huu wa kuinua akina mama kiuchumi. Hadi kufikia tarehe 30/05/2015 kiasi cha Tshs 37,492,500/= sawa na asilimia 78.8 tayari kimerejeshwa

Halmashauri ya Wilaya katika bajeti ya mwaka 2015/2016 imetenga kiasi cha Tshs. **45,647,600**/= kwa ajili ya kuvikopesha vikundi 14 mbalimbali vya vijana kupitia SACCOS ya Vijana kutokana na azma hiyo ya kuinua vijana kiuchumi kwa mwaka 2015/16.

## **9 ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA**

### **Mafanikio:-**

- Elimu juu ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 8 imetolewa kwa mwaka 2005 hadi 2015 zoezi hili ni endelevu.
- Jumla ya viwanja **828** vimepimwa Biharamulo Mjini na Nyakanazi na ujenzi wa majengo mbalimbali unaendelea.
- Uhifadhi wa vyanzo vya maji umeongezeka kutoka vyanzo vya maji **280** mwaka 2005 hadi kufikia vyanzo vya maji **360** mwaka 2015 sawa na asilimia **29**
- Matukio ya uchomaji moto yamepungua kwa asilimia **30**, kutoka asilimia **80** mwaka 2005 hadi asilimia **50** mwaka 2015;
- Jumla ya miche ya miti **15,291,000** imepandwa kati ya mwaka 2005 na 2015 na jumla ya miti **14,285,000** sawa na asilimia **93.4** ya miti yote iliyopandwa imepona na inaendelea kukua vizuri;

- Matumizi ya mizinga ya kisasa na kiasili yameongezeka kutoka mizinga **471** mwaka 2005 hadi mizinga **1,632** mwaka 2015 sawa na asilimia **246**
- Uzalisha wa asali na nta kwa mwaka 2005 ulikuwa Kg **97,764.3** yenye thamani ya Tshs **58,658,580/=** na kg **391.7** za nta yenye thamani ya Tshs **1,175,100/=**. Mwaka 2015 uzalishaji wa asali ulikuwa ni kg **977,643** yenye thamani ya Tshs **586,585,800** sawa na ongezeko la uzalishaji wa asilimia **900** na nta kg 3,917 yenye thamani ya Tshs **11,751,000**
- Uandaaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi mwaka 2005 haukufanyika katika vijiji na mwaka 2014/2015 mpango umefanyika katika Vijiji **8** vya; Isambara, Nyabusenzi, Kasato, Ntumagu, Katahoka, Runazi, Kagondo na Kalenge.
- Hatimiliki za ki-mila ziliandaliwa **0** mwaka 2005 na mwaka 2014/2015 hatimiliki **1,272** ziliandaliwa kwa wananchi wenye mashamba husika.
- Mwaka 2005 kulikuwa na Masijala za ardhi **0** na mwaka 2015 Wilaya ina masijala za ardhi za vijiji **9** kati yake masijala **3** zimejengwa na **6** zimekarabatiwa

## **10 ELIMU**

Ibara ya 85 (a-g) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 inaelekeza kuboresha, kuimarisha na kupanua elimu bora katika ngazi zote.

Katika kuboresha elimu ya msingi na sekondari sekta ya elimu imepata mafanikio katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2015 kama ifuatavyo:-

### **10.1 Elimu ya Awali:**

Mwaka 2005 wilaya ilikuwa na shule za Awali **26** zenye jumla ya wanafunzi **745** wavulana **412** na Wasichana **333**. Hadi kufikia mwaka 2015 shule za Awali zimeongezeka na kufikia shule **88** zenye jumla ya wanafunzi **11,704** Wavulana **5,991** na Wasichana **5,713** sawa na ongezeko la asilimia **238**.

## **10.2 Elimu ya Msingi:-**

Uandikishaji wanafunzi darasa la Kwanza umeongezeka kutoka watoto **4,988** mwaka 2005 hadi kufikia wanafunzi **18,751** mwaka 2014/2015 sawa na ongezeko la asilimia **276**.

Idadi ya shule za msingi imeongezeka toka Shule **70** mwaka 2005 hadi kufikia shule **88** mwaka 2015. Kati ya hizo **85** ni za serikali, **3** ni za binafsi/mashirika sawa na ongezeko la asilimia **26**.

Idadi ya wanafunzi wa darasa la I-VII katika shule za Serikali imeongezeka kutoka wanafunzi **30,746**(wavulana **15,101**, wasichana **15,645**) mwaka 2005 hadi kufikia wanafunzi **56,905** (wavulana **28,577**, wasichana **28,328**) mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia **85%**

Idadi ya walimu kwa mwaka 2005 ilikuwa **401** hadi mwaka 2015 Wilaya ina jumla ya walimu **1532** walimu wa kike **566** na walimu wakiume **966**. Hata hivyo bado kuna mahitaji ya walimu 248 hii imetokana na uwingi wa wanafunzi wanaosajiliwa kuingia darasa la kwanza.

Uwiano wa walimu kwa wanafunzi umeboreka kutoka **1:63** mwaka 2005 hadi **1.56** mwaka 2015 ambao ni chini ya malengo ya Kitaifa (MKUKUTA) ya **1:45**.

Idadi ya nyumba za walimu zimeongezeka kutoka **84** mwaka 2005 hadi nyumba **213** kwa mwaka 2015. Mahitaji ni kuwa na Nyumba **841**





Ujenzi wa nyumba za walimu Shule ya Msingi Mkunkwa

Kwa mwaka 2005 uwiano wa kitabu kwa wanafunzi ulikuwa **1.4** na kwa mwaka 2015 uwiano wa kitabu kwa wanafunzi (BPR) umeboreka kufikia uwiano 1:3 hivyo lengo la kitabu **1:1** bado halijafikiwa

Uwiano wa madawati kwa wanafunzi umeboreka kutoka dawati **1:5** mwaka 2005 hadi kufikia dawati **1:4** mwaka 2015

Kiwango cha ufaulu kwa mtihani wa darasa la saba kimepanda kutoka asilimia **72.5** mwaka 2006 hadi asilimia **89.14** mwaka 2014. Kwa matokeo hayo wilaya imeshika nafasi ya pili kitaifa kwa miaka miwili mfululizo;

Idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza imendelea kubaki asilimia 100 kutoka mwaka 2006 hadi asilimia **100** mwaka 2014.

Sababu kubwa iliyochangia kufikia asilimia 100 ni pamoja na;-

- Jitihada kubwa zinazofanywa na walimu kutoa elimu bora na kuhakikisha walimu wanakamilisha mtaala kwa wakati
- Kuboreka kwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia kunakofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo Wilayani.

### Jedwali 5: linaloonyesha ufaulu kwa mwaka 2006 hadi 2015

MWA KA	WALIOSAJILIWA			WALIOFANYA MTIHANI			%	WALIOFAULU			%	WALIOCHAGULIWA A KUIINGIA KIDATO CHA I			%
	ME	KE	JML	ME	KE	JML		ME	KE	JML		ME	KE	JML	
2006	255 5	1878	<b>443 3</b>	253 6	184 5	<b>438 1</b>	98.8 27	236 1	158 0	<b>3941</b>	89.957	236 1	1580	<b>394 1</b>	100
2007	116 2	742	<b>190 4</b>	113 6	720	<b>185 6</b>	97.4 79	100 9	539	<b>1548</b>	83.405	100 9	539	<b>154 8</b>	100
2008	209 9	2032	<b>413 1</b>	206 3	199 2	<b>405 5</b>	98.1 6	157 0	222 3	<b>3793</b>	93.539	157 0	2223	<b>379 3</b>	100
2009	204 5	2170	<b>421 5</b>	204 4	217 0	<b>421 4</b>	99.9 76	184 0	195 3	<b>3793</b>	90.009	184 0	1953	<b>379 3</b>	100
2010	142 6	1538	<b>296 4</b>	139 0	148 7	<b>287 7</b>	97.0 65	108 5	100 1	<b>2086</b>	72.506	108 5	1001	<b>208 6</b>	100
2011	122 2	1253	<b>247 5</b>	119 1	112 7	<b>231 8</b>	93.6 57	979	927	<b>1906</b>	82.226	979	927	<b>190 6</b>	100
2012	139 0	1540	<b>293 0</b>	133 2	149 0	<b>282 2</b>	96.3 14	111 7	119 5	<b>2312</b>	81.928	111 7	1195	<b>231 2</b>	100
2013	133 3	1358	<b>269 1</b>	128 9	132 0	<b>260 9</b>	96.9 53	113 3	110 0	<b>2233</b>	85.588	113 3	1100	<b>223 3</b>	100
2014	138 0	1389	<b>276 9</b>	132 8	135 2	<b>268 0</b>	96.7 86	121 6	117 3	<b>2389</b>	89.142	121 6	1173	<b>238 9</b>	100
2015	141 8	1546	<b>296 4</b>												

#### Chanzo : Mkurugenzi Mtendaji (W)

Vyumba vya Madarasa kwa mwaka 2005 vilikuwa **350** hadi mwaka 2015 vimeongezeka na kufikia vyumba **599** ikiwa ni ongezeko la vyumba **249** sawa na asilimia **71**. Hata hivyo bado kuna upungufu wa vyumba vya madarasa **837**

Matundu ya vyoo kwa mwaka 2005 vilikuwa **477** na kwa mwaka 2015 vyoo vimekuwa **1,169**. Ongezeko la matundu ya vyoo **692** sawa na asilimia **145**.

### **10.3 Elimu ya Sekondari:**

Wilaya imepata mafanikio makubwa katika utoaji wa huduma ya elimu ya sekondari katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi juni 2015 kama ifuatavyo:-

- Wilaya ya Biharamulo ina Shule **20** za Sekondari, kati ya hizo Shule **18** ni za Serikali na shule **2** za dhehebu la dini.
- Idadi ya shule za serikali imeongezeka kutoka **3** mwaka 2005 hadi **18** mwaka 2015 sawa ongezeko la asilimia **500**;
- Idadi ya shule zisizo za serikali imeongezeka kutoka **1** mwaka 2005 hadi **2** mwaka 2015 sawa na asilimia **100**.
- Shule za Sekondari za Serikali zenye “A Level”zimeongezeka kutoka **0** mwaka 2005 hadi **5** mwaka 2015.
- Shule za sekondari zisizo za serikali zenye “A Level” imebakia kuwa mmoja (**1**) tangu mwaka 2005 hadi mwaka 2015. Shule hiyo inaitwa Katoke Seminari
- Vyumba vya maabara vimeongezeka toka vyumba 2 mwaka 2005 hadi vyumba 15 mwaka 2015 na vyumba 39 vipo hatua mbalimbali za ujenzi
- Aidha Wilaya ina Wanafunzi **8,756** wakiwemo Wavulana **5,340** na Wasichana **3,416**. Kuna Walimu **630** wakiwemo wanaume **398** na wanawake **232**. Wilaya ina upungufu wa Walimu **72** wa sayansi.
- Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi ulikuwa **1:50** kwa mwaka 2005, hadi mwaka 2015 uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi ni **1:13**
- Vyumba vya madarasa vimeongezeka kutoka **71** mwaka 2005 hadi **151** mwaka 2015 sawa na asilimia **113**
- Hosteli zimeongezeka kutoka **0** mwaka 2005 hadi **14** mwaka 2015
- Idadi ya walimu imeongezeka kutoka **85** mwaka 2005 hadi **667** mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia **685**

### **10.4 Ufaulu wa Mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha Pili mwaka 2005 - 2015**

Mwaka 2005 jumla ya wanafunzi **320** walioandikishwa kufanya mtihani (Wavulana**168** na Wasichana **152**). Waliofanya mtihani walikua Jumla ya wanafunzi **320** (Wavulana**168** na Wasichana **152**.) Waliofaulu walikua Jumla ya wanafunzi **285** (Wavulana**150** na Wasichana **135**) sawa na

asilimia **89** Walioshindwa walikuwa Jumla ya wanafunzi **35** (Wavulana **18** na Wasichana **17**.)

Mwaka 2010 jumla ya wanafunzi **1685**(wavulana **957**, wasichana **728**) walijiandikisha kufanya mtihani wa kumaliza kidato cha pili. Waliofaulu walikuwa **1302**(wavulana **766**, wasichana **536**), walioshindwa walikuwa **383** (wavulana **191**, wasichana **192**)

Mwaka 2014 jumla ya wanafunzi **1,256** walioandikishwa kufanya mtihani (Wavulana **668** na Wasichana **588**). Waliofanya mtihani walikua Jumla ya wanafunzi **1,256** (Wavulana **668** na Wasichana **588**.) Waliofaulu walikua Jumla ya wanafunzi **1,112** (Wavulana **636** na Wasichana **456**) sawa na asilimia **89** Walioshindwa walikuwa Jumla ya wanafunzi **85** (Wavulana **32** na Wasichana **53**)

### **10.5 Ufaulu wa Mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha Nne mwaka 2005-2015**

Mwaka 2005 jumla ya wanafunzi **271**(wavulana **143** na wasichana **128**) walijiandikisha kufanya mtihani wa kidato cha nne. Wanafunzi waliopata daraja la I ni **10** (wote wavulana), daraja II walikuwa **36**( wavulana **25**, wasichana **11**). Daraja la III walikuwa **54**(wavulana **31**, wasichana **23**), daraja la IV walikuwa **80**(wavulana **27**, wasichana **53**), Walioshindwa walikuwa **60** (wavulana **35** na wasichana **25**) na ambao hawakufanya mtihani walikuwa **31**(wavulana **15**, wasichana **16**)

Mwaka 2014 jumla ya wanafunzi **687** (wavulana **394**, wasichana **293**) walijiandikisha kufanya mtihani. Wanafunzi waliopata daraja la I walikuwa **38**(wavulana **31**, wasichana **7**), daraja II walikuwa **74**(wavulana **43**, wasichana **31**), daraja la III walikuwa **124**(wavulana **83**, wasichana **41**), daraja la IV walikuwa **257**(wavulana **145**, wasichana **112**) Walioshindwa walikuwa **180**(wavulana **85**,wasichana **95**) na ambao hawakufanya mtihani walikuwa **14**(wavulana **7** , wasichana **7**)

## **10.6 Elimu ya Ualimu:-**

Kwa mwaka 2005 hapakuwa na chuo cha Ualimu na kwa mwaka 2015, Wilaya ina Chuo **1** cha Ualimu cha Nyamahanga kinachomilikiwa na dhehebu la Kipentekoste.

## **10.7 Elimu ya Ufundi:-**

Mwaka 2005 wilaya ilikuwa na vyuo **2** (kabla ya kuanzishwa Wilaya ya Chato) na kwa mwaka 2015 Wilaya ina vyuo vya ufundi viwili (**2**) (Chuo cha Maendeleo ya Wananchi – Rubondo na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi wa magari – Biharamulo Vocation Training Center). Lengo kuu ni kutoa elimu ya kuwawezesha vijana kujitegemea na kujiajiri katika fani mbalimbali.

## **11 AFYA**

Ibara ya 86 (a–m) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inaelekeza kuboresha huduma za Afya. Na kwa kuzingatia pia malengo ya millennia lengo namba 4,5 na 6 yanayosema kwamba ;kupunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka 5, kuboresha huduma za afya za uzazi na kudhibiti UKIMWI,Malaria, na magonjwwa mengineyo. Kwa kuzinga malengo hayo wilaya imepata mafanikio kama ifuatavyo;-

- Zahanati zimeongezeka kutoka **15** mwaka 2005 hadi **24** mwaka 2015; kati ya hizo **3** ni za Mashirika ya Dini na **2** ni za watu binafsi sawa na ongezeko la asilimia **60**;
- Vituo vya afya vimeongezeka kutoka **2** mwaka 2005 hadi **5** mwaka 2015 vituo vyote vinamilikiwa na Serikali, ambavyo ni Nyabusozzi, Nyakanazi, Rukaragata, Kalenge na Nyakahura sawa na ongezeko la asilimia **150**



#### Ujenzi wa jengo la upasuaji Kituo cha afya Kalenge

- Hospitali imebaki kuwa 1 hadi sasa ambayo inamilikiwa na dhehebu la dini.
- Kiwango cha wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya na kuhudumiwa na wahudumu wenye mafunzo zimeongezeka kutoka asilimia **48.2** mwaka 2005 hadi asilimia **68** mwaka 2015
- Vifo vya akina mama wajawazito (katika vizazi 100,000) vimepungua kutoka **105/100,000** mwaka 2005 hadi **68/100,000** mwaka 2015

#### ***11.1 Chanjo za watoto chini ya mwaka mmoja zimeongezeka kama ifuatavyo:-***

- Polio (kutoka **78%** mwaka 2005 hadi **91.6%** mwaka 2014);
  - BCG (kutoka **89.3%** mwaka 2005 hadi **97.9%** mwaka 2014);
  - DPT HB (kutoka **80.6%** mwaka 2005 hadi **93.4%** mwaka 2014);
  - Pepopunda kwa wajawazito kutoka **70.5%** mwaka 2005 hadi **89.9%** kwa mwaka 2014);
  - Surua (kutoka **81%** mwaka 2005 hadi **91%** mwaka 2014).
- Vifo vya watoto wachanga (IMR) chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka **16/1000** (2005) hadi **3/1000** (2014);

- Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka **23/1000** mwaka 2005 hadi **9/1000** mwaka 2014 sawa na asilimia **61**;
- Vyandarua **27,525** vyenye dawa ya kuua mbu viligawiwa kwa akina mama wajawazito na **15,668** viligawiwa kwa watoto chini ya miaka mitano.
- Kaya **42,924** kati ya **44,164** sawa na asilimia **97.2** zilipuliziwa dawa ya ukoko ya kuua mbu waenezo ugonjwa wa malaria
- Maambukizi ya ugonjwa wa malaria katika jamii yamepungua kutoka wagonjwa **156/1,000** mwaka 2005 hadi **122/1,000** kufikia mwaka 2014

Uwepo wa watumishi wa Afya.

- Waganga (Madaktari, Tabibu na Tabibu wasaidizi) walikuwa **36** mwaka 2005 hadi **45** mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia **25**;
- Wauguzi na wahudumu wa afya walikuwa **102** mwaka 2005 hadi **271** mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia **166**;



Jengo la ofisi ya Mganga mkuu wa wilaya

## ***11.2 Upatikanaji wa Dawa na Vifaa vya Tiba***

Upatikanaji wa Dawa na vifaa vya tiba kwa mwaka 2005 ni wa kuomba kulingana na mahitaji ya kituo kutokana na magonjwa yaliyopo maeneo husika (ILS) pia MSD wanasafirisha Dawa hadi kituo vya tiba. Pia Mfumo wa DRF unasaidia upatikanaji wa dawa katika vituo vyote vya tiba.

## ***11.3 UKIMWI***

Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI yamepungua kutoka asilimia **10.8** mwaka 2005 hadi asilimia **3.2** mwaka 2015;

Wagonjwa wanaopata matibabu ya dawa za ARV wameongezeka kutoka **230** mwaka 2005 hadi **3,863** mwaka 2014

Watu waliojitokea kupima afya zao kwa hiari wameongezeka kutoka **1,859** mwaka 2005 hadi **97,920** mwaka 2015

Vituo vya utoaji ushauri nasaha na dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (CTC) vimeongezeka kutoka **2** mwaka 2005 hadi **11** mwaka 2015. Pia kuna huduma ya tohara kama kinga ya HIV inayotolewa katika kituo cha afya bila malipo yoyote

## **12 Ustawi wa Jamii**

### ***12.1 Ukomeshaji wa ajira kwa watoto***

Suala la ajira kwa watoto sio kubwa katika Halmashauri yetu hasa baada uboreshaji wa elimu ya msingi kupitia programu ya MEM na programu ya elimu sekondari (MMES). Programu hizo zimesaidia kuandikisha watoto wanaliokuwa na umri wa kwenda shule na kumaliza elimu ya msingi na kuendelea na elimu ya sekondari baada ya serikali kujenga shule ya sekondari kila kata. Pia baada ya kuwaondoa wachimbaji wadogo katika eneo la moja moja na West zone kule Mavota na kupungua upatikanaji wa madini ya dhahabu katika eneo la Busiri. Bado tuna himiza jamii kuwapa watoto haki zao za msingi ili watoto wasikimbilie



kutafuta vibarua. Jamii itaendelea kuhimizwa kuwalea watoto na kuwasaidia wale wanao ishi katika mazingira hatarishi.

### ***12.2 Watoto walemavu***

Jumla ya watoto 22 (wakiume 14 na wakike 8) wenye ulemavu wa ngozi walikuwa wametambuliwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2014/2015. Halmashauri imewapeleka watoto hawa katika maeneo yenye ulinzi Mugeza S/M na Kituo cha Kabanga Kasulu kwa ajili ya malezi, makuzi na kuwapatia fursa ya masomo. Kati ya watoto hao watoto 16 (Me - 10 na Ke - 6) wako katika Shule Maalum ya Mugeza iliyoko wilaya ya Bukoba. Watoto 6 (Me - 4 na Ke - 2) pamoja na wazazi/walezi wao wamepelekwa katika kituo cha Malezi ya watu wenye ulemavu cha Kabanga, wilayani Kasulu. Kwa wale wanao soma katika shule ya Mugeza, sehemu kubwa ya mahitaji yao yanagharamiwa na Halmashauri ya wilaya.

### ***12.3 Watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi***

Hadi kufikia juni 2015 jumla ya watoto 6513 (**Ke** - 3193 na **Me** - 3320) walioko katika mazingira hatarishi walikuwa wametambuliwa kutoka kata zote 15.

Idadi ya watoto wanaosomeshwa na Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeongezeka kutoka watoto 380 (**Ke** - 108 na **Me** - 172) mwaka 2010/2011 hadi watoto 784 (**Ke** - 376 na **Me** - 408) mwaka 2014/2015. Halmashauri kwa upande wake imeendelea kugharamia nauli za kwenda na kurudi shuleni pamoja na kuwalipia ada baadhi ya wanafunzi walio na uhitaji mkubwa. Jumla ya wanafunzi 46, (wakiwemo 19 wakike na 27 wa kiume) wamelipiwa ada kufikia mwaka 2014/15 ikilinganishwa na wanafunzi **40** (**Ke** - 14 na **Me** - 16) waliolipiwa ada mwaka 2010/2011.

Wadau wa maendeleo wametoa mchango mkubwa kwa kusaidia juhudi za Halmashauri katika kuwasaidia watoto walio katika mazingira hatarishi kama ifuatavyo;

- Kampuni ya African Barrick kupitia uliokuwa mgodi wa TULAWAKA ambao ulifadhili wanafunzi **38** kusoma katika chuo cha VETA Shinyanga.

- Kanisa la Anglican (Tumaini Fund) lilipa ada kwa ajili ya wanafunzi 374 (**Ke-179** na **Me-195**) katika shule 18 za sekondari kwa gharama ya Tshs. 7,480,000. Kwa upande wa misaada kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kufanya Mitihani, Tumaini Fund iliwezesha wanafunzi 257 (**Ke-113** na **Me-144**) wa kidato cha pili kufanya mitihani yao, kwa gharama ya Tshs. 2,570,000/= . Pia kiasi cha Tshs. 9,850,000/= kilitolewa na shirika hili kuwezesha wanafunzi 197 (**Ke-78** na **Me-99**) wa kidato cha nne kufanya mitihani yao kufikia mwaka 2014/2015.

Mkakati kuhakikisha ulinzi na usalama kwa watu wanaoishi katika Mazingira Hatarishi vijijini ikiwa pamoja na walemavu wa ngozi umeishatolewa kwa Watendaji wa Kata na vijiji kwa utekelezaji. Mkakati huo ni

- a) Vijiji na vitongoji vyote vitoe ulinzi wa kutosha kwa watu wenye ulemavu, kwa njia ya ulinzi shirikishi hususan kwa kuwashirikisha Vijana waaminifu na kuweka utaratibu wa kuwawezesha kadiri itakavyoonekana inafaa;
- b) Maafisa Watendaji wa Vijiji waanzishe, watunze na kutumia daftari la utambuzi wa wageni wote wanaofika kijijini, au kitongojini ili matendo yao yaweze kudhibitiwa; **Daftari hilo ni budi lioneshe:**  
Tarehe mgeni alipofika kijijini, Jina kamili la Mgeni, Jina la mwenyeji wake, Uhusiano wake na Mwenyeji wake, Sababu za kufika hapo kijijini, Jina la kitongoji cha mwenyeji wake, Jina la Mwenyekiti wa kitongoji hicho, Muda ataokaa hapo kijijini na Tarehe ya kuondoka.
- c) Utamaduni uliokuwapo hapo nyuma, wa kuwauliza na kuwahoji wageni wote wasiofahamika kijijini ufufuliwe na kuzingatiwa kikamilifu,
- d) Namba za simu za OCD/OC-CID Biharamulo na RPC/RCO, zilitolewe kwa ajili ya kusaidia na kurahisisha mawasiliano kati ya watu wenye ulemavu wa ngozi na vyombo vya dola endapo wataona mazingira yanayotia mashaka.

## **12.4 Wazee**

Wilaya yetu inaendelea kufanya utambuzi wa wazee katika vijiji na kata zote. Kufikia mwezi Juni 2015 jumla ya wazee 4343 kutoka katika kata 10, walikuwa wametambuliwa wakiwa katika makundi yafuatayo:

<b>UMRI</b>	60 - 70	71 - 80	81+	<b>JUMLA</b>
<b>IDADI YA WAZEE</b>	2797	1084	462	4343

### **Chanzo: Ofisi ya mkurugenzi Mtendaji (W)**

Kwa sasa Wilaya inaadhimisha siku ya wazee kila tarehe 01, Oktoba ya kila mwaka. Halmashauri imeweka utaratibu wa kuwapatia matibabu wazee wote huduma za Afya bila ya malipo. Katika utaratibu huo wazee wametengenezewa vitambulisho maalumu ili viweze kuwasaidia wanapohitaji huduma ya afya katika Hospitali, vituo vya afya na zahanati zote hapa Wilayani. Jumla ya wazee 1,016 tayari wamepatiwa vitambulisho.

## **13 MAJI:**

Ibara ya 87 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005-2015 inaelekeza kuendeleza programu ya maendeleo sekta ya maji.

### **13.1 Huduma ya Maji Safi na Usafi wa mazingira**

Kitaifa Serikali iliweka malengo ya kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wakazi wa mjini kwa asilimia **90** ilikapo mwaka 2015. Upatikanaji wa maji Kitaifa katika miji ni **75%**.

Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya maji ni kama ifuatavyo:-

- Kumekuwa na ongezeko la miradi ya maji ya visima virefu kutoka **0** mwaka 2005 hadi **83** mwaka 2015
- Visima vifupi vimeongezeka kutoka **80** mwaka 2005 hadi **446** kufikia mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia **458**.
- Miradi ya bubujiko (gravity schemes) imeongezeka kutoka **1** mwaka 2005 hadi **7** mwaka 2015 sawa na asilimia **600**.
- Mitambo ya kusukuma maji kutoka **2** mwaka 2005 hadi mitambo **8** mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia **300**.
- Idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama vijijini imeongezeka kutoka asilimia **29** mwaka 2005 hadi asilimia **62** mwaka 2015;
- Idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama mjini imeongezeka kutoka asilimia **31** mwaka 2005 hadi asilimia **68** mwaka 2015;

- Utekelezaji wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji ulianza na vijiji **10** kwa kuanza na hatua ya usanifu ambao ulikamilika tangu mwaka 2011. Hatua ya ujenzi wa miundombinu ya maji vijiji 10 kwa sasa chini ya mkakati wa tekeleza kwa matokeo makubwa sasa BRN unaendelea na baadhi imeshakamilika .

**Jedwali na 6: hali halisi ya utekelezaji kimaumbile kwa sasa**

<b>Mradi</b>	<b>Malengo</b>	<b>Utekelezaji</b>	<b>% Utekelezaji</b>	<b>Maoni</b>
<b>1.</b> Visima virefu kijiji cha Kasato	Ujenzi wa visima virefu 10	Visima vimekamilika 10	100	Vina tumika
<b>2.</b> Visima virefu kijiji cha Kagondo	Ujenzi wa visima virefu 10	Visima vimekamilika 10	98	Kisima 1 bado kufungwa pampu
<b>3.</b> Visima virefu kijiji cha Kasozibakaya	Ujenzi wa visima virefu 10	Visima vimekamilika 9	90	Kisima 1 kilikosa maji ,
<b>4.</b> Visima virefu na vifupi kijiji cha Nyabusozzi	Ujenzi wa visima virefu 10 na vifupi 20	Visima virefu vimekamilika, visima vifupi vimechimbwa 10 17	90	Uchimbaji na ujenzi wa visima vifupi 20 umesimama
<b>5.</b> Visima virefu na vifupi kijiji cha Nyantakara	Ujenzi wa visima virefu 8 na vifupi 15	Visima virefu vimekamilika 7 Visima vifupi vimejengwa bado 15 pump	90	Ufungaji wa pampu umesimama ukisubiri malipo
<b>6.</b> Mradi wa maji Mabare /Mihongora	Ujenzi vituo vya maji 46, ukarabati tanki 1(135m3) , Ujenzi wa tank 1(90m3), bomba km56, Lambo la maji, Nyumba ya mtambo, mashine ya maji , mfumo wa kutibu wa maji	Ujenzi wa muiundombinu yote imekamilika	100	Wananchi kupitia uongozi wao wanakataa mradi .uendeshaji umesimama
<b>7.</b> Mradi wa maji Nyakanazi	Ukarabati wa mradi wa maji ya bomba kwa kulaza mabomba km 4.7,	chanzo cha maji kimejengwa na vituo vya maji (DP 17	42	Kazi imesimama

	Kijenka tenki chini ya aridhi 75m <sup>3</sup> , ufungaji wa mtambo, nyumba ya mtambo	)vimejengwa. Mabomba ya maji km 2.5 yamelazwa , ujenzi wa pump house upo hatua ya umaliziaji,kazi bado kukamilika. ununzi wa bomba za chuma		
8.Mradi wa maji Bisibo	Ujenzi wa mradi wa bomba, DP 18, kisima kirefu mtaro wa maji km 22.25, nyumba ya mtambo, uwekaji wa pampu	uchimbaji wa mtaro km 13, ujenzi wa tanki la maji 130m3 (95%), utafiti wa kisima kirefu na ujenzi wa DPs 10	35	Kazi imesimama
9.Mradi wa maji Katoke	Ujenzi wa mradi wa maji ya bomba, DP 15, Mtaru wa maji km 12.25, kisima kirefu 1 , nyumba ya mtambo na kufunga pampu1, tanki la maji 90m3	mtaro umechimbwa km 12.25, ujenzi wa DP 11, utafiti wa kisima kirefu, ujenzi wa DPs 10, ujenzi wa tanki 90m3 (95%)	35	Ujenzi umesimama

### Chanzo : Mkurugenzi Mtendaji (W)

Mradi wa maji ya kijiji cha Mabare/Mihongora Kata ya Nyakahura na Mradi wa maji ya kusukumwa kwa nguvu Kijiji cha Nemba Kata ya Nemba



## 14 MIUNDOMBINU:

### 14.1 Sekta ya Barabara

Wilaya ya Biharamulo kwa mwaka 2005 ilikuwa na mitandao wa Barabara km 53.4 Mpaka kufikia mwaka juni 2015 kuna mtandao wa Barabara zenye urefu wa km 715, kati ya hizo km. 372 ni za Mkoa, Km 343 ni za Wilaya. Kati ya kilometa hizo km 210 ni barabara za lami. Kilometa 543 ni za changarawe

**Jedwali Namba 7 Fedha za matengenezo ya barabara zilizotolewa na Halmashauri pamoja na Serikali kuu toka mwaka wa fedha 2005/2016 hadi mwaka, 2014/2015**

<b>S/N</b>	<b>MWAKA WA FEDHA</b>	<b>UREFU (Km)</b>	<b>KALVATI / MADARAJA</b>	<b>KIASI (Tshs)</b>
1	2005 /2006	53.4		62,284,000.00
2	2006 / 2007	23	2	42,472,000.00
3	2007 / 2008	131	9	158,740,000.00
4	2008 / 2009	106	18	222,441,750.00
5	2009 / 2010	117.8	14	217,992,000.00
6	2010 / 2011	101		305,500,000.00
7	2011 / 2012	153		430,200,000.00
8	2012 / 2013	167		545,300,000.00
9	2013 / 2014	198	1	1,000,008,000
10	2014 / 2015	244	216	856,500,000.00
				<b>3,841,437,750.00</b>

**Chanzo : Mkurugenzi Mtendaji (W)**

Katika ibara ya 64 – 67 ya Ilani ya Uchaguzi ya C.C.M. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya hii ni kama ifuatavyo:-

- Wilaya ina mtandao wa Barabara zenye urefu wa kilomita **343** kati ya hizo kilomita **1.2** imejengwa kwa kiwango cha lami;
- Asilimia ya barabara za Wilaya zilizo katika hali nzuri na ya kuridhisha imepanda kutoka asilimia **75** mwaka 2010 na kufikia asilimia **85** mwaka 2015.
- Wilaya pia inazo barabara za mkoa na za kitaifa zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) zenye jumla ya kilometa 372. Kati ya hizo km. 120 ni za lami (Ngara border – Geita border) na km. 90 za kiwango cha lami (Kasindaga – Biharamulo – Lusahunga). Barabara hizo zinatumiwa kusafirisha mazao ya shambani na kupeleka pembejeo za kilimo maeneo ya kilimo kwa urahisi zaidi.



Barabara ya lami Mgurukani hadi Boma lodge.



Ujenzi wa daraja la Nyampalahala linalounganisha Wilaya za Biharamulo na Chato

## **14.2 UMEME:**

### **i. Umeme.**

Huduma ya nishati ya Umeme kupitia Shirika la ugavi wa umeme (TANESCO) katika Wilaya ya Biharamulo ilianza Novemba mwaka 2004 katika mji wa Biharamulo na vitongoji vyake kwa kutumia mashine **2** zinazofanya kazi kwa pamoja. Hadi kufikia mwaka 2010 wateja walikuwa wamefikia 250. Katika kipindi cha kuanzia 2010 hadi sasa wateja wameongezeka na kufikia 3,127. Idadi hii inatarajiwa kuongezeka na kufikia wateja 5,127 mara tu utakapo kamilika mradi wa REA ambao kwa sasa vijiji vitakavyounganishwa ni kumi (Nyamahanga, Lusahunga, Kabindi, Nyakahura, Nyakanazi, Katahoka, Ntungamo, Nyambale, Rwagati na Runazi).



### **14.3 Mawasiliano ya Simu.**

Idadi ya Makampuni yanayotoa huduma ya simu imeongezeka kutoka makampuni kutoka Kampuni moja (1) TTCL mwaka 2005 hadi makampuni matano mwaka 2014/2015. (Makampuni hayo ni TTCL, Voda Com, Airtel, Tigo na Zantel)

## **15 UKUSANYAJI WA MAPATO:**

- Katika kipindi cha 2005 hadi 2015 Halmashauri ya Wilaya imeendelea kupokea fedha kutoka Serikali kuu na wahisani mbali mbali na zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2005 kiasi kilicho pokelewa ni Tshs 9,827,614.45 wakati kiasi kilichopokelewa 2014/2015 ni Tshs 14,655,661,448.32
- Kuanzia kipindi cha 2005 Halmashauri ya Wilaya yetu imeweza kusimamia kikamilifu makusanyo ya mapato yake kama ilivyo ainishwa katika bajeti zake na kiwango cha ukusanyaji kimeongezeka kutoka Tshs 288,893,300 mwaka 2005 hadi Tshs 1,175,905,201.02 mwaka 2014/2015 sawa na ongezeko la asilimia 307.

### **Ukaguzi wa Hesabu za Serikali**

Halmashauri imeweza kuandaa taarifa za mahesabu za kila mwaka na kuwasilisha TAMISEMI na kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa wakati na kwa mujibu wa sheria. Wilaya pia imeweza kujibu hoja zote zilizo tolewa na Mkaguzi wa ndani na Mkaguzi Mkuu wa serikali kwa wakati uliopangwa.

Aidha Halmashauri imeweza kufunga hesabu za Halmashauri kwa wakati na kwa mafanikio makubwa ambapo Halmashauri imeweza kupata HATI SAFI kwa miaka 8 mfululizo kama inavyoonekeana kwenye jedwali hapa chini;-

### **Jedwali Na.12: Ukaguzi wa hesabu za Serikali**

<b>Mwaka</b>	<b>Hati iliyotolewa</b>
--------------	-------------------------

2006/2007	Hati safi
2007/2008	Hati safi
2008/2009	Hati safi
2009/2010	Hati safi
2010/2011	Hati safi
2011/2012	Hati safi
2012/2013	Hati safi
2013/2014	Hati safi

**Chanzo : Mkurugenzi Mtendaji (W)**

## 16. ULINZI NA USALAMA

Hali ya Ulinzi na Usalama Wilayani kwetu kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2010 hadi sasa imekuwa ni ya kuridhisha. Hata hivyo yapo matukio yaliyojitokeza na mengine kudhibitiwa na Jeshi la Polisi likishirikiana na vyombo vingine vya dola pamoja na Wananchi. Kwa muhtasari jedwali hapo chini linaonyesha matukio ya uhalifu huo:

**Jedwali Na. 1: HALI YA MATUKIO KUTOKA MWAKA 2010 HADI 2015**

<b>Na.</b>	<b>Matukio</b>	<b>2010</b>	<b>2011</b>	<b>2012</b>	<b>2013</b>	<b>2014</b>	<b>2015</b>	<b>Jumla</b>
1.	Mauaji ya Albino	-	-	-	-	-	-	-
2.	Mauaji ya Vikongwe	-	17	14	03	17	01	51
3.	Unyang'anyi wa kutumia silaha	1	10	11	05	03	-	30
4.	Utekaji wa magari	-	06	04	04	-	-	14
5.	Wizi wa Mifugo	2	98	53	07	106	20	262
6.	Kupatikana na madawa ya kulevya (bangi)	1	10	16	04	17	01	47
		<b>4</b>	<b>141</b>	<b>98</b>	<b>23</b>	<b>123</b>	<b>22</b>	<b>385</b>

Kutokana na takwimu hizo inaonesha kuwa makosa ya mauaji yamepungua kwa kiwango cha kuridhisha hususan mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino) na Vikongwe kwa imani za kishirikiana baada ya

kufanya operesheni maalum kuwa baina waganga wanaopiga ramli chonganishi na upigaji wa mara kwa mara wa kura za siri kuwabaini wahalifu.

## **17 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUITATUA**

Changamoto kuu zinazokabili Wilaya na Mpango wa kuzikabili kwa miaka 5 ijao ni kama ifuatavyo:

- i. **Changamoto:** Upungufu wa vituo vya kutolea huduma za Afya ukilinganisha na idadi ya Wakazi waliopo;

**Mkakati:** Halmashauri imehamasisha kila Kijiji kianze na ujenzi wa Zahanati na tayari jumla ya zahanati 24 zimekamilika na zinatoa huduma na zahanati 3 ujenzi upo hatua mbalimbali.

- ii. **Changamoto:** Watu walio wengi wanaoishi na VVU na UKIMWI kushindwa kuwa wazi na tatizo walilionalo kwa kuogopa kunyanyapaliwa na Jamii hivyo kushindwa kupata huduma inayostahili;

**Mkakati:** Halmashauri inaendelea kutoa elimu ya kupunguza unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI kwa njia ya semina, warsha na mikutano;

- iii. **Changamoto:** Upungufu wa vitendanishi (reagents and test kits) mfano “Determine strips and unigold” kwa ajili ya upimaji wa VVU;

**Mkakati:** Halmashauri inaendelea kuwasiliana na Bohari ya madawa ya Kanda (MSD) na wadau mbalimbali kama vile ICAP ili vifaa hivyo viweze kupatikana mapema.

- iv. **Changamoto:** Gharama za uendeshaji wa huduma za maji kibiashara kuwa kubwa. Mfano ankra ya umeme kwa mwezi

ni kiasi cha Tshs. **5,600,000/=**, gharama nyingine za uendeshaji zinagharimu kiasi cha Tshs. **10,800,000/=** kwa mwezi ukilinganisha na mapato yatokanayo na makusanyo ya mwezi ya Tshs **8,000,000/=** kutokana na uchakavu wa mtandao wa mabomba;

**Mkakati:**

- Halmashauri inaendelea kusimamia vizuri mapato yanayotokana na uuzaji wa huduma hiyo na pia utafutaji wa vyanzo vya maji vingine unaendelea kufanyika;
- Halmashauri imetenga kiasi cha tshs 60,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa pampu ili kuboresha usambazaji wa maji Biharamulo mjini na kupunguza gharama za umeme ambapo pampu iliyopo inatumia umeme mwingi kuliko kiwango cha maji kinachosukumwa na pampu .

v. **Changamoto:**

Katika sekta ya elimu ya msingi wilaya inazo changamoto za miundombinu ya vyumba ya madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na madawati kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 8 Miundo mbinu shule za msingi**

Na.	Aina	Mahitaji	Yaliyopo	%	Upungufu	%
1	Vyumba vya madarasa	1,436	599	41.71	837	58.29
2	Nyumba za walimu	841	213	25.33	628	74.67
3	Matundu ya vyoo	2,584	1,169	45.24	1,415	54.76
4	Madawati	32,295	14,584	45.16	17,711	54.84

Chanzo : Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

## ELIMU SEKONDARI

Wilaya inazo changamoto za miundombinu ya vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo, majengo ya utawala, mabweni, maktaba na mabwalo kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

### Jedwali Na 9 Miundo mbinu ya shule za sekondari

Na	Aina	Mahitaji	Yaliyopo	%	Upungufu	%
1.	Vyumba vya madarasa	227	151		76	
2.	Nyumba za walimu	228	70		158	
3.	Vyoo	449	339		110	
4.	Majengo ya utawala	18	8		10	
5.	Mabweni	38	14		24	
6.	Maktaba	45	9		36	

#### Chanzo: Mkurugenzi Mtendaji (W)

- Upungufu wa walimu 72 wa masomo ya sayansi (Fizikia 20, Kemia 20, na Biologia 32).

**Mkakati:** Mikakati iliyopo katika kukabiliana na changamoto hizi ni pamoja na kuendelea kuhamasisha na kuhimiza wananchi na Wadau wengine kuchangia katika ujenzi wa Nyumba za Walimu, Vyumba vya Madaarasa, Maabara, Hosteli, Vyoo na samani.

Aidha Wilaya imeendelea kuhamasisha Taasisi na watu Binafsi kujenga na kuendesha Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyu.

- vi. **Changamoto:** Changamoto kubwa inayozikabili SACCOS zilizopo ni pamoja na upugufu wa Mtaji. Wanachama waliojiunga wana uwezo mdogo wa kujenga mtaji unaohitajika ili kuendesha SACCOS hizo, na kutokana na hali hiyo SACCOS zimekuwa tegemezi kwenye Taasisi za fedha kama Benki na Taasisi nyingine za fedha ambazo masharti ya mikopo yao ni magumu, ikiwa ni pamoja na kuwa na riba kubwa, gharama za mkopo ziko kiasi cha juu sana na hata zikifanikiwa kupata mkopo, mikopo hiyo haitoki kwa wakati. Pamoja na jitihada kubwa wanazofanya wanachama za kuzalisha kwa kutumia

mikopo wanayoipata lakini sehemu kubwa ya faida imekuwa ikirudi kwenye asasi hizo kama gharama za mkopo badala ya kuwasaidia kupunguza umasikini;

**Mkakati:** Halmashauri inaendelea kuhamasisha wanachama ili waongeze akiba, amana na hisa ili waweze kujenga mtaji wao;

- vii. **Changamoto:** Eneo linalolimwa kuwa dogo, vile vile tija kwa wakulima kwa Mazao makuu ya Biashara na Chakula bado ni ya kiwango cha chini. Aidha jitihada/**Mikakati** ya kuongeza eneo linalolimwa na kuongeza tija, zinafanyika kama ifuatavyo:
- Ili kuondokana na kilimo cha kutengemea jembe la mkono linalochangia kulima eneo dogo, matumizi ya wanayamakazi katika Kilimo yameendelea kutiliwa mkazo ikiwa ni pamoja na matumizi ya Matrekta madogo na makubwa

viii. **Ukosefu wa Mitaji kwa Wakulima:**

**Mkakati:** Katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa mitaji kwa wakulima, Wilaya inaendelea kuwashauri wananchi kujiunga kwenye SACCOS ili waweze kunufaika na utaratibu wa kukopa kutoka Taasisi mbalimbali za fedha. Aidha idara ya ushirika itaendelea kutoaji wa elimu kwa vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) na kufanya ukaguzi wa hesabu kila mwaka

ix. **Ulinzi na Usalama**

**Changamoto zinazokabili Jeshi la Polisi ni kama ifuatavyo:**

- a. Uhaba wa vitendea kazi hasa magari na pikipiki.
- b. Upungufu wa Raslimali Watu na vifaa.
- c. Hali ya kijiografia ya wilaya yetu ambapo sehemu kubwa ni misitu

**Mikakati ya Kudhibiti Uhalifu.**

Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola na Wananchi wameendelea kutekeleza yafuatayo:

- a. Kuimarisha vituo vya ukaguzi (check point) kwenye barabara za Biharamulo – Muleba katika pori la Kasindaga, barabara ya Lusahunga – Nyakahura eneo la ngazi saba, na kituo cha ukaguzi kingine kimoja kipo katika barabara ya Nyakanazi – Kalenge
- b. Doria za magari na pikipiki kwenye barabara za Lusahunga – Bukoba, Nyakahura – Nyakanazi na Nyakanazi – Kibondo.
- c. Kuimarisha kikosi cha intelijensia pia kuhusisha na kuendeleza michezo kwa vijana na pia kuwashirikisha wananchi kwenye suala zima la ulinzi na usalama kupitia vikundi vya ulinzi shirikishi vilivyopo katika vijiji vyote 80 Wilayani.

### **Wahamiaji haramu.**

Tunalo tatizo kubwa la wahamiaji haramu kama lilivyo kwenye Wilaya nyingine za Mkoa wa Kagera. Wilaya yetu inao Wahamiaji wengi wanaovutiwa na mazingira, ambao hutumia misitu yetu ya hifadhi kama sehemu ya maficho na malisho ya mifugo, Kilimo na upasuaji wa mbao usio rasmi. Wengi wa wahamiaji hao wanatokea nchi za jirani za Rwanda, Burundi na Uganda.

Wahamiaji haramu 79 walipewa hati za kufukuzwa nchini (P.I. Notice) kama ifuatavyo; Raia wa Burundi 142, Raia wa Rwanda 36 na Raia wa Uganda 09 na Kenya 01. Wahamiaji haramu 26 kutoka mataifa ya Rwanda 17 na Burundi 09 walipelekwa Mahakamani kwa kosa la kuishi nchini kinyume cha sheria. Kati ya hao wahamiaji 9 walifungwa (Rwanda 4 na Burundi 5). Wahamiaji 17 (Burundi 11 na Rwanda 6) walirejeshwa makwao.

### **Changamoto;**

- i. Elimu/uelewa mdogo wa Wananchi na viongozi wa vijiji na vitongoji wa ngazi za chini juu ya madhara ya wahamiaji.
- ii. Jiografia ya Wilaya hasa mapori ambapo wahamiaji haramu hujificha na kufanya vitendo vya kihalifu.

**Mikakati ya kukabiliana na Wahamiaji Haramu.**

- (i) Tunaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala yote yahasuyo uhamiaji kupitia viongozi wa ngazi zote.
- (ii) Vitabu maalum (daftari) 15 vimesambazwa kwa ajili ya kuorodhesha wahamiaji wote katika kata zote 15 za Wilaya kwa lengo la kuendelea kuwabaini, kuwatambua mahali waliopo na shughuli wanazozifanya.

Imetolewa:

Kitengo cha Habari na mawasiliano.